JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 1055, ARUSHA
Simu : (027) 2503538/ 2507928
Nukushi : (027) 2505973
Barua pepe:rbcarusha@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

ARUSHA - MEI, 2023

UDHIBITI WA UPOTEVU WA MAPATO WAPANDISHA MAKUSANYO KATIKA MNADA WA LOCIRWA WILAYANI MONDULI

Mojawapo wa Majukumu ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) chini ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 Marekebisho ya 2019, kifungu cha 7(a) na (c) ni kufanya uchambuzi wa mifumo ya kiutendaji katika maeneo mbalimbali ili kuboresha namna ya utendaji katika eneo husika na kushauri namna ya kuziba mianya ya rushwa kadiri inavyobainika. TAKUKURU inatekeleza jukumu hili kupitia Kurugenzi ya Uzuiaji Rushwa.

1.0 UZUAJI RUSHWA
1.1 SUCCESS STORY

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Arusha kupitia Ofisi yake ya Wilaya ya Monduli katika utekelezaji wa jukumu la uzuiaji rushwa ilifanya uchambuzi wa Mfumo wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ushuru wa mifugo katika mnada wa LOCRWA. Uchambuzi ulibaini ng'ombe hulipiwa ushuru wa Tshs. 7,500/= kila mmoja, Tshs. 3,000/= kwa kila mbuzi na Ths. 3,000/= kwa kila kondoo. Awali kabla ya uchambuzi, mapato yaliyokuwa yanapatikana kwa siku ya mnada (Alhamisi) yalikuwa yanafikia kiasi cha Tshs. 3,000,000/=.

Moja kati ya changamoto zilizobainika katika ukusanyaji wa ushuru utokanao na mauzo ya mifugo katika mnada tajwa ni pamoja na uchache wa wakusanyaji wa ushuru ukilinganisha na ukubwa wa eneo la Mnada, na wakusanya ushuru kukaa kwenye kituo kwa muda mrefu hali iliyosababisha kuzoeleka katika eneo hilo. TAKUKURU ilipendekeza mambo kadhaa ikiwemo ushuru huo kukusanywa na Mgambo. Baada ya utekelezaji wa maazimio hayo, mapato katika mnada huo kulinganisha na makusanyo ya siku za nyuma yaliongezeka; **Mfano kwa tarehe 16.03.2023 yalipanda hadi kufikia Tshs. 6,200,000/= kutoka Tshs. 3,000,000/= kwa siku za nyuma.**

Aidha TAKUKURU Mkoa wa Arusha katika utekelezaji wa jukumu la uzuiaji rushwa, ilifanya ufuatiliaji wa mradi wa barabara ya St. James yenye urefu wa kilometa 0.5 na barabara nyingine zilizoko kwenye mradi huo kwa lengo la kuhakikisha thamani ya fedha inafikiwa katika utekelezaji wa mradi huo. Pamoja na barabara hiyo kukamilika kwa viwango vilivyokusudiwa, ilijitokeza changamoto ya ajali za mara kwa mara hasa kwa wanafunzi ambao ni watumiaji wakubwa wa barabara hiyo ya St. James. Kijiografia barabara hiyo inapita pembeni mwa jengo la Ofisi ya TAKUKURU (M) Arusha.

Kutokana na kupungua kwa usalama wa waenda kwa miguu katika barabara hiyo, Ofisi ilifanya uchambuzi uliojikita katika eneo la "Hali ya Usalama" wa barabara hiyo ili kubainisha sababu za kuwepo kwa ajali za mara kwa mara. Uchambuzi ulibaini sababu mojawapo kubwa ni kukosekana kwa kivuko au kizuizi cha kuwafanya waendesha vyombo vya moto kupunguza mwendo ili kuruhusu wenda kwa miguu kuvuka. Ili kukabiliana na hali hiyo, TAKUKURU ilifanya kikao na Wadau wa barabara (TARURA) na kukubaliana kuweka TUTA na alama ya punda milia (ZEBBRA CROSSING). Kazi hiyo ilifanyika kwa ufanisi na kwa sasa barabara hiyo ni salama kwa waenda kwa miguu ambao wengi ni wanafunzi wa shule ya Msingi na Sekondari Kaloleni, shule ya msingi Makumbusho.

1.2 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Katika kipindi tajwa jumla ya **miradi 21** yenye thamani ya **Tshs. 8,567,266,288.06** ilifuatiliwa na TAKUKURU Mkoa wa Arusha. Kati ya miradi hiyo, **Mradi mmoja** wenye thamani ya **Shs. 74,102,884** ulikutwa na kasoro kubwa na hatua kuchukuliwa kama inavyooneshwa katika jedwali:

S/N	KITUO	ORODHA YA MIRADI ILIYOBAINIKA KUWA NA KASORO	THAMANI YA MIRADI (shs)	YALIYOBAINIKA	HATUA ZILIZO CHUKULIWA NA TAKUKURU
1.	Arusha	01 Ujenzi wa kivuko cha waenda kwa Miguu Mtaa wa Engosengiu Awamu ya kwanza	Tsh. 74,102,884	Hakuna thamani ya fedha. Fundi wa kupasua mwamba alipatikana bila kufuata utaratibu. Mzabuni wa vifaa upatikanaji wake haukuzingatia kanuni za manunuzi ya umma 2013.	Uchunguzi ulianzishwa kupitia majalada PCCB/AR/RB/16/ 2023 & PCCB/AR/RB/17/ 2023

				Mzabuni wa vifaa amelipwa na hajafikisha vifaa kwenye mradi.	
JUMLA		01	Tsh. 74,102,884		

1.3 UCHAMBUZI WA MIFUMO

S/N	KITUO	IDADI YA YA CHAMBUZI ZA MIFUMO	LENGO LA CHAMBUZI ZA MIFUMO	YALIYOBAINIKA	MAKUBALI ANO
1	Arusha	03	Uchambuzi wa mfumo wa hali ya usalama wa watumiaji wa barabara ya St James, Kata ya Kaloleni, Halmashauri ya Jiji la Arusha	Kutokuwepo kwa miundombinu za tahadhari kwa watumiaji wa barabara	TARURA waweke miundombinu za tahadhari kwa watumiaji wa barabara kama vile zebra, matuta n.k (Zimewekwa)
			Uchambuzi Wa Madeni Ya Vikundi, Vicoba Na Saccos Yatokanayo Na Mikopo Ya 10% Ya Mapato Ya Halmashauri Ya Jiji La Arusha	Ufuatiliaji mdogo wa madeni, urejeshaji wa kusuasua kwa madeni, uhifadhi mbovu wa kumbukumbu za vikundi vilivyo kopa.	Halmashauri iimarishe ufuatiliaji wa madeni ya vikundi pamoja na uhifadhi wa taarifa.
2	Longido	00	Warsha ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa kutumia POS H/Longido	Fedha za makusanyo kuchelewa kuingizwa kwenye akaunti, Mikataba ya mawakala wa makusanyo kutokukidhi vigezo, Control namba za malipo kutolewa kwa kuchelewa,	Halmashauri iimarishe mfumo mzima wa makusanyo ya mapato ie: mikataba ya mawakala wa makusanyo, POS zitolewe kwa maandishi, control namba

				POS kutolewa bila makabidhiano ya kimaandishi, Changamoto za upatikanaji wa taarifa za mawakala na vibarua wa makusanyo,	zitolewe kwa wakati, Halmashauri ianzishe utaratibu wa kuwapima mawakala kwa mkataba wa nyuma kabla ya kutoa mkataba mpya. Uhifadhi wa taarifa za vibarua wa ukusanyaji uimarishwe.
4	Monduli	05	Uchambuzi wa mfumo wa Usimamizi wa masoko	Idadi ndogo ya wakusanyaji wa mapato inayo athiri kiasi cha mapato yanayo kusanywa.	Halmashauri itumie mgambo kwenye ukusanyaji wa mapato
			Uchambuzi kuhusu upotevu wa mapato ya Vijiji kijiji cha Orkeeswa	Vijiji vingi vina akaunti sinzia, Vijiji havina POS, Baadhi ya vijiji vina watendaji wanaokaimu ambao sio watumishi wa Umma.	Akaunti za vijiji zifufuliwe, Halmashuari ihakikishe mapato yanakusnywa kwa POS Mkurugenzi aombe kibali cha ajira na watendaji wan aokaimu wawe watumishi,

			Uchambuzi wa mfumo wa ujenzi na usimamizi wa miradi inayosimamiwa na shule ya Shikizi Lolera	Usimamizi duni wa miradi kutokana na umbali wa shule shikizi. Kutekeleza miradi bila kamati. Usimamizi mbovu wa Halmsahauri. Shida ya maji kwenye miradi	kamati zitekeleze majukumu yake, kuimarisha usimamizi wa mradi kwa kutumia watendaji wa kata, sserikali ya kijiji ihakikishe upatikanaji wa maji kwenye mradi
			Uchambuzi wa mfumo wa utekelezaji na usimamizi wa miradi ya TARURA Wilaya ya Monduli	Hakuna ushirikishwaji wa wananchi kwenye utekelezaji wala uibuliwaji wa mradi.	TARURA kuanzia ngazi ya Mkoa washirikishe wananchi katika uibuliwaji wa miradi,
5	Karatu	03	Kutathmini mianya ya rushwa kwenye • Uidhinishaji fomu za uchunguzi wa matibabu kwa wanafunzi kituo cha Afya Karatu	Utozwaji wa fedha ambazo haziingii kwenye mfumo wa serikali, na bila kutumia mashine za POS	Halmashauri wataingiza ununuzi wa mashine hizo kwenye bajeti. Kwa sasa tayari wanatumia vitabu kuhifadhi kumbukumbu za malipo.

			• Usimamizi wa utoaji leseni za biashara karatu	Uwepo wa wafanyabiashara wanaoendesha shughuli zao bila kuwa na TAX Clearence ya TRA, kwa hiyo hawana leseni	Elimu itolewe kuhusu uzingativu wa kufanya utakaso wa kodi kwa wafanya biashara
			Tathmini ya hatari ya Rushwa katika usimamizi wa mazao ya misitu Wilaya ya Arumeru.	Adhabu zitolewazo kwa wahalifu wa mazao ya misitu ni ndogo	Bado.
6	Ngoro ngoro	02	Uchambuzi wa Mfumo wa Makisio na ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri ya wilaya ya Ngorongoro	Makisio yako chini, Uwajibikaji mdogo kwenye makusanyo, Mianya ya rushwa kwenye makusanyo	Wadau wakutane ili kuanisha vyanzo vya mapato & kuboresha ukusanyaji, Kuweka mkakati wa makusanyo
			Tathmini ya hatari ya Rushwa katika usimamizi wa mazao ya misitu wilaya ya Ngorongoro.	Uvunaji usio zingatia sheria, Hakuna vizuia, Upungufu wa rasilimali watu & vitendea kazi,	Viwekwe vizuia vya mazao ya misitu, Rasilimali watu na vitendea kazi viongezwe.

2.0 TAKUKURU RAFIKI

TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA TAKUKURU RAFIKI (TR) KWA KIPINDI CHA FEBRUARI NA MACHI 2023 NGAZI YA MKOA WA ARUSHA					
MKOA	**IDADI YA KATA ZILIZOFIKIWA**	**IDADI YA KERO ZILIZOTOLEWA**	**IDADI YA KERO ZILIZOTATULIWA**	**MIFANO YA KERO KISEKTA NA NAMNA ZLIVYOTATULIWA**	**MAFANIKIO YA TR KATIKA MKOA WAKO KWA KIFUPI**
Arusha	12	95	35	• Malipo makubwa ya ulinzi kwa wafanyabiashara wa Soko **UTATUZI:** Makubaliano yaliwekwa kila meza italipiwa Shs. 1,000/- kwa mwezi, badala ya Shs. 300/- kwa siku iliyokuwa inalipwa awali • Vibanda vya soko kushikiliwa na watu wasiovitumia huku wengine wakiwa hawana na kulazimika kuweka bidhaa chini. **UTATUZI:** Mkurugenzi wa Jiji alielekezwa kuhakiki vibanda vyote visivyotumika na kuvigawa kwa watu wengine wenye uhitaji • Banda bovu kutokurekebishwa kwa wakati na kutishia usalama wa watu na mali zao.	• Kuweza kupata ufumbuzi wa haraka kwa kero ndogndogo za wananchi • Kuwawezesha wananchi kupata jukwaa la kueleza changamoto zao • Kuwakutanisha wananchi na wadau muhimu wa shughuli za maendeleo katika maeneo yao • Wananchi kuona Seirikali inawathamini kwa kuwapa nafasi ya kuwasikiliza

				UTATUZI: Mkurugenzi wa Jiji la Arusha alifahamishwa na kulifanyia banda husika marekebisho na kwa sasa linatumika • Bill kubwa za maji na wakati mwingine kuletewa bill ya maji hata kama maji hayatoki. **UTATUZI:** Afisa wa AUWSA aliwaelimisha wananchi kuwa bill kubwa za maji mara nyingi zinasababishwa na ubovu wa miundombinu ambayo husababisha maji kuvuja. Hivyo aliwashauri wananchi kufuatilie hali ya miundombinu yao ya maji na kuhakikisha kuwa iko salama muda wote ili kuepuka uvujaji wa maji.	

3.0 UELIMISHAJI UMMA:

Na	KAZI	UFAFANUZI
1.	Elimu kwa Viongozi, Watendaji na Watumishi wa Sekta ya Umma na Binafsi kwa lengo la kuwawezesha kutambua wajibu wao katika Kuzuia vitendo vya Rushwa.	Elimu ya Kuzuia Rushwa iliendelea kutolewa kwa Makundi haya muhimu kwa njia ya semina na kuwapa fursa ya kutoa maoni yao njia sahihi inayoweza kutumika kudhibiti vitendo vya rushwa katika sekta ya Umma na Binafsi.
		Jumla ya Semina 26 ziliendeshwa
2.	Kutembelea na kuimarisha Klabu za Wapinga Rushwa katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo.	Kuwajenga vijana Kimaadili mojawapo ya jukumu endelevu la TAKUKURU Mkoa wa Arusha ambapo wanachama wa klabu za wapinga rushwa wameelimishwa na kushirikishwa katika shughuli mbalimbali ili

		kuwawezesha kushiriki katika kutambua na kuzuia vitendo vya rushwa katika maeneo yao. **Jumla ya klabu za wapinga rushwa 57 ziliimarishwa.**
3.	Kuwashirikisha Wananchi katika Mapambano dhidi ya Rushwa kupitia Mikutano ya Hadhara.	Wananchi kwa makundi mbalimbali katika mkoa wa Arusha walielimishwa juu ya athari za rushwa na kuhamasishwa kushirikiana na Serikali katika Kudhibiti vitendo vya rushwa. Uelimishaji huo ulifanyika kwa njia ya Mikutano ya Hadhara ambapo kwa kipindi tajwa **Jumla ya Mikutano ya Hadhara 31 ilifanyika.**

Pia, Elimu dhidi ya Rushwa ilitolewa kupitia Vipindi vya Redio **04**, Maonesho **03** na Uandishi wa Habari **03**

4.0 UCHUNGUZI NA MASHTAKA

Katika kipindi tajwa jumla ya taarifa **169** kwa njia mbalimbali, ambapo taarifa za **rushwa ni 128** na **zisizo za rushwa ni 41**. Mchanganuo wa taarifa hizo kisekta ni kama ifuatavyo: -

4.1 UCHUNGUZI

4.1.1 MCHANGANUO WA TAARIFA KISEKTA

Na	SEKTA	IDADI YA TAARIFA
1	Afya	5
2	Ardhi	11
3	Maji (AUWSA)	4
4	Biashara	4
5	Benki	8
6	Halmashauri	65
7	Kilimo	4
8	Mazingira	6
9	Miradi ya Maendeleo	3
10	Polisi	6
11	TASAF	1
12	Ujenzi (TARURA, TANROADS)	7
13	Utalii	1
14	Vikundi	5
15	Mahakama	8
16	Elimu	9
17	Ulinzi	6
18	Ajira	3

19	NSSF	1
20	Madai	11
21	TPHPA (Viatilifu)	1
	JUMLA	**169**

MCHANGANUO WA TAARIFA ZINAZOHUSU RUSHWA NA AMBAZO SIO ZA RUSHWA

KITUO	TAARIFA ZA RUSHWA	TAARIFA ZISIZO ZA RUSHWA
ARUSHA	73	29
ARUMERU	12	03
MONDULI	18	03
LONGIDO	08	00
KARATU	06	03
NGORONGORO	11	03
JUMLA	**128**	**41**

Taarifa (**128**) zenye viashiria vya rushwa chunguzi zake zimeinzishwa na ziko katika hatua mbalimbali. Aidha kwa taarifa (**41**) zisizo za rushwa wahusika walishauri idara sahihi za kwenda kupata utatuzi wa shida zao na taarifa hizo zimefungwa.

N.B. Taarifa zisizo za Rushwa ni 24.26%

4.2 MASHTAKA

S/Na	KITUO	KESI MPYA	KESI ZILIZOSHINDA	KESI ZILIZOSHINDWA
1	ARUSHA	06	01	00
2	ARUMERU	01	00	00
3	MONDULI	00	02	00
4	LONGIDO	01	00	00
5	KARATU	00	00	00
6	NGORONGORO	00	00	00
	JUMLA	**08**	**03**	**00**

5.0. USHIRIKIANO NA WADAU

Katika hatua nyingine, TAKUKURU Mkoa wa Arusha imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake na majukumu ya Taasisi nyingine za serikali na Binafsi kwa lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora bila vikwazo vyote.

Miongoni mwa wadau ambao TAKUKURU Mkoa wa Arusha imeshirikiana nao ni: -

S/N	JINA LA MDAU	ENEO LA USHIRIKIANO	MAFANIKIO
1.	MAHAKAMA	Uendeshaji wa mashauri ya rushwa yanayofikishwa mahakamani kwa wakati	Ukamilishaji wa mashauri na hatua kuchukuliwa kwa wakati
2.	MWENDESHA MASHTAKA WA SERIKALI (NPS)	Kufanya vikao vya mara kwa mara vya kiutendaji na vya kujadili maendeleo ya chunguzi na mashauri yaliyopo mahakamani	Kurekebisha kasoro zote katika chunguzi kabla ya kufikisha mashauri Mahakamani
3.	HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA	Upatikanaji wa Ushahidi wa Maelezo na Vielelezo katika tuhuma zinazoendelea Mahakamani	Ukamilishaji wa chunguzi na watuhumiwa kufikishwa Mahakamani kwa wakati e.g kesi zinazohusu watuhumiwa katika ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mashine za maalumu (POS)
4.	OFISI YA MKUU WA WILAYA YA ARUSHA	Kukagua na kufanya ufuatiliaji katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Halmashuri ya Jiji la Arusha	Ufanisi katika utekelezaji wa miradi umeanza kuonekana hasa katika miradi iliyokuwa imekwama, kwa sasa inaendelea kutekelezwa Mfano ni Ujenzi wa OPD katika hospitali ya Wilaya ya Arusha na Kituo cha Afya Mkonoo.

6.0 MAADHIMISHO YA WIKI YA SHERIA

S/N	TAREHE	KAZI ILIYOFANYIKA	WADAU TULIOSHIRIKIANA NAO
1.	22.01.2023	Kushiriki maandamano ya uzinduzi wa Wiki ya Sheria Jijini Arusha	Mahakama na Wadau wote wa Mahakama
2.	22-27.01.2023	Kutoa elimu kwa njia ya Maonesho katika viwanja vya TRA -Arusha	Mahakama na Wananchi
3.	24 – 27.01.2023	Kutembelea shule za msingi na sekondari (Naurei, Kaloleni, Kilimanjaro Muslim na Ilboru) kwa ajili ya kutoa elimu ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa	Mahakama, TAWLA, POLISI
4.	23.01.2023	Kuelimisha Wazee wa Mila na wananchi Kata ya Monduli Juu kuhusiana na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa	Viongozi wa Mila, Wananchi
5.	24 & 26.01.2023	Kuendesha vipindi vya radio	Mahakama
6.	27.01.2023	Kutembelea Magereza kwa ajili ya kutoa elimu na kusikiliza kero zao	Mahakama, NPS, KDU, POLISI
7.	30.01.2023-01.02.2023	Kushiriki maandalizi na sherehe ya kilele cha maadhimisho ya wiki ya sheria	Mahakama na Wadau wake
8.	28.01.2023	Kushiriki Bonanza la kuhitimisha wiki ya sheria	Mahakama Wadau wake

7.0 MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

S/N	TAREHE	KAZI ILIYOFANYIKA	WADAU TULIOSHIRIKIANA NAO
1.	07.03.2023	Kutembelea na kutoa mahitaji muhimu kwa Watoto wenye uhitaji wa kituo cha 'Kindness Children's Centre'.	Kindness Children's Centre
2.	08.03.2023	Kushiriki Maandamano na Mkutano katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.	Idara ya maendeleo ya Jamii Mkoa na wilaya, Wanawake wa Idara na Taasisi za Serikali na binafsi za Jijini Arusha.

8.0 MIKAKATI YA APRILI JUNI 2023

TAKUKURU Mkoa wa Arusha, katika robo ya Aprili hadi Juni, 2023 imejipanga kutekeleza kwa utaratibu Programu ya TAKUKURU RAFIKI ili kupata fursa ya kuwafikia wananchi na wadau, kushirikiana nao katika Kuzuia vitendo vya rushwa katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na upatikanaji wa Huduma za Kijamii. Jukumu hili litafanywa na TAKUKURU kwa kuwashirikisha kwa karibu Viongozi, Watendaji na Wadau wote katika ngazi ya Kata zilizopo Mkoa wa Arusha.

Programu hii ya TAKUKURU RAFIKI itaenda sanjari na utoaji elimu kwa makundi husika juu ya Madhara ya Rushwa na namna wanavyoweza kushikiana na TAKUKURU katika kudhibiti vitendo vya rushwa.

Aidha, TAKUKURU Mkoa wa Arusha itaendelea kupokea na kufanyia chunguzi malalamiko ya vitendo vya rushwa na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria wale wote watakaobainika kujihusisha na ubadhirifu na ufujaji wa fedha za umma, ili kuokoa fedha za Serikali zinazoelekezwa katika shughuli mbalimbali za Maendeleo.

9.0 WITO

Nitumie nafasi hii kutoa rai kwa Wananchi na Wadau wote wa Mkoa wa Arusha kuendelea kushirikiana na TAKUKURU Mkoa wa Arusha kwa kujiepusha na vitendo vya rushwa na kutoa taarifa kwa wakati pale wanapoona viashiria vya rushwa katika maeneo yao. Kila Mwananchi atambue kwamba miradi ya maendeleo inayotelezwa na serikali au wafadhili katika maeneo yao ni kwa manifaa yao, hivyo kila mmoja awajibike kuifahamu na kufuatilia utekelezaji wake ili kuweza kubaini kasoro kwa wakati na kuzitolea taarifa zitakazowezesha

hatua kuchukuliwa kwa wakati kuepusha upotevu wa fedha unaoweza kusababisha miradi hiyo kukwama.

Aidha wananchi watumie mbao za matangazo katika ofisi za Kata na Mitaa yao kupata taarifa za miradi inayotekelezwa katika maeneo yao na kuifuatilia kwa karibu.

"Kuzuia rushwa ni Jukumu Lako na Langu, Tutimize Wajibu wetu"

Imetolewa na:

Zawadi Ngailo;

KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M);

Simu: 0738 150 064